TANGAZO LA SERIKALI NA. 81 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (USHURU WA HUDUMA) YA HALMASHAURI YA MJI WA HANDENI YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 367 la 2019

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Huduma) ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ya Mwaka 2024, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Huduma) ya Halmashauri ya Mji wa Handeni ya Mwaka 2019 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya aya ya 4

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya aya ya 4 kama ifuatavyo:

"Ushuru wa huduma

4. Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kutoka kwa mtu yeyote anayefanya biashara kwa kutumia leseni ya biashara kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu ya mauzo gafi ya ongezeko la Kodi ya Ongezeko Thamani kutokana na uzalishaji wa bidhaa, kazi na huduma zinazofanyika ndani ya eneo la Halamashauri".

Lakari ya Halmashauri ya Mji Handeni imegongwa kwenye Sheria ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji ya uliofanyika tarehe 07 Mwezi February mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya:-

MARYAM A. UKWAJU
*Mkurugenzi wa Halmashauri,*
*Halmashauri ya Mji Handeni*

MUSSA A. MKOMBATI
*Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Mji Handeni*

NAKUBALI

L.S

Dodoma
9 Disemba, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa*